# BRIGHT VISION SERIES
## DARASA LA NANE - MWAKA - 2023
SASON 001
## KISWAHILI : LUGHA

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

I) JINA LAKO    II) JINA LA SHULE YAKO    MUDA: SAA 1 DAK. 40

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaid kati ya yale uliyopewa.***

Tatizo kuu __1__ wananchi wengi ni __2__ ya juu ya maisha ambayo __3__ na ukame na athari ya COVID-19 __4__ mambo mengine.

Wazazi wengi __5__ na mzigo wa ulipaji karo na mahitaji __6__ ya kimsingi wamejikuta katika njia panda. Aidha kuna wale __7__ chakula cha siku moja __8__ maji ya matumizi ya nyumbani au mifugo yao. Hata hivyo hawakukosea waliposema __9__ yaani kila jambo huwa na mwisho wake.

1. A. linalowakubali B. inayowakabili C. linalowakabili D. linalokabidhiwa
2. A. maisha B. gharama C. wajibu D. mpango
3. A. imesababisha B. zimesababishwa C. yamesababisha D. imesababishwa
4. A. miongoni mwa B. baina ya C. zaidi ya D. karibu na
5. A. wamelewa B. wamelemewa C. wamefaulu D. wamefurahia
6. A. mingi B. nyingi C. wengi D. mengi
7. A. wasiyoweza B. kishoweza C. wasioweza D. wasiyeweza
8. A. wala B. bali C. ila D. na
9. A. hakuna nyongeza mbaya B. hakuna refu lisilo na ncha C. bendera hufuata upepo D. ukishikwa shikamana

Shairi ni __10__ maalum __11__ maudhui __12__ kumhusu mwanadamu na __13__ zake katika mazingira __14__. Shairi __15__ beti, mishororo, mizani, vina na vibwagizo.

10. A. hadithi B. mtungo C. habari D. methali
11. A. wenye B. yenye C. zenye D. lenye
12. A. ambao B. ambayo C. ambaye D. ambalo
13. A. umbo B. vitendo C. mambo D. hulka
14. A. anayoishi B. anaoishi C. anamoishi D. anakoishi
15. A. ina B. zina C. lina D. una

***Kuanzia swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Tulifika shuleni saa 7:45. Ni sawa na
    A. saa moja na robo
    B. saa nane kasorobo
    C. saa mbili kasorobo
    D. saa saba na dakika arubaini na tano
17. ***Tumia 'amba';-***
    Aliyenisaidia ndiye huyu
    A. Ambaye aliyenisaidia ni huyu
    B. Ambaye alinisaidia huyo
    C. Ambaye alionisaidia ni huyu
    D. Ambaye alinisaidia ndiye huyu
18. Chagua orodha ambayo hailingani
    A. Lo, salaale, eboo, lahaula
    B. Aghalabu, pale, yupi, hodari
    C. Wewe, mimi, sisi, yeye
    D. Zetu, wake, langu, wao
19. ***Kanusha;-*** Mwanafunzi aliyetuzwa ni huyu
    A. Mwanafunzi aliyetuzwa si huyu
    B. Mwanafunzi asiyetuzwa ni huyu
    C. Mwanafunzi asiyetuzwa si huyu
    D. Mwanafunzi ambaye alituzwa si huyu
20. Chagua jibu lisilo na maana sawa na 'panda"
    A. ongezeka
    B. paramia mti kwenda juu
    C. pembe kubwa yenye tundu nchani
    D. ruka kutoka sehemu moja hadi nyingine
21. Chagua sentensi isiyo na kivumishi cha pekee.
    A. Mwenye macho haambiwi tazama
    B. Nyumba nyingine imejengwa mjini
    C. Mtoto mtiifu alizawadiwa jana
    D. Wengine waliruhusiwa kuenda nyumbani
22. Chagua sentensi iliyotumia kiunganishi sahihi
    A. ikiwa watu ambao hujitahidi hufaulu
    B. vitabu vyote vimeletwa maadamu kimoja
    C. tulichoka sana almuradi hatukupumzika
    D. licha ya kuwa na baridi hawakuvaa mavazi mazito
23. Ni sentensi gani iliyo katika wakati uliopo?
    A. Tulichelewa kufika shuleni
    B. Ninasoma kitabu cha "siku njema"
    C. Naimba wimbo wa taifa
    D. Yeye hucheza kandanda ughaibuni
24. ***Kitendawili;-***
    Mlango ni wangu mna askari
    A. kufuli  B. kivuli
    C. bawabu  D. moyo
25. Angekuwa na uwezo angetusaidia, ni sawa na kusema
    A. alitusaidia ilhali hakuwa na uwezo
    B. hakutusaidia iwapo alikuwa na uwezo
    C. hakutusaidia japo hakuwa na uwezo
    D. hakutusaidia maadamu hakuwa na uwezo
26. Chagua methali isiyoambatana na zile zingine
    A. damu ni nzito kuliko maji
    B. abebwaye hujishika
    C. ushikwapo shikamana
    D. ukibebwa usilevyelevye miguu
27. Ni pambo lipi halivaliwi sikioni?
    A. Kipini  B. Kipuli
    C. Mapete  D. Herini
28. Chagua sentensi sahihi kisarufi.
    A. Sisi wote tulifika mapema
    B. Yeye hujitahidi katika masomoni yake
    C. Angeliona gari hilo angeondoka
    D. Ng'ombe ambaye aliyechinjwa ni wake
29. Chagua kiwakilishi katika sentensi.
    Wote watiifu walipokea vyeti vyao jana.
    A. Wote  B. Watiifu
    C. Vyao  D. Jana
30. Mti ulianguka ukavunjika
    A. ka!  B. pu!
    C. keche!  D. tiki!

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia 31 - 40.***

Ama kwa hakika wahenga hawakukosea walipoamba kuwa kumcha Mungu si kilemba cheupe. Methali hii inasisitiza kuwa kutii na kutenda wema sio lazima uonekane na ujulikane na kila mtu kuwa u mzuri ilhali katika undani wako ni mbwamwitu na hivyo basi ukawa umevalia ngozi ya kondoo. Nilielewa ukweli wa methali hii kwa njia mbaya.

Siku zilizidi kuyoyoma na maisha yakaendelea vyema, nilikuwa napendwa sana na wazazi wangu. Kila nilichotaka walikuwa tayari kufanya juu chini ili nisikose, sikujua kumbe nilikuwa na starehe za mbwa kukalia mkia wake. Starehe zangu zilikuwa za muda mfupi sana kwani, yatendekayo gizani hubainika bayana kwenye mwangaza.

Kumbe chochote king'aacho si dhahabu u umdhaniye ndiye siye. Ndugu yangu alionekana mtoro na mtundu sana lakini kama nilivyoelewa ni kuwa aliishi maisha yaliyostahili. Mimi niliyatenda mambo yasiyofaa na kuyafunika ili yasijulikane. Nilionekana kama mtu ambaye ni mcha Mungu sana hivyo basi kuzighilibu roho za watu walionipenda katika kiombo cha panda shuka. Naangamia ilhali dadangu yu mzima kama kigongo. Siku moja nilimdanganya mama yangu kuwa tuna mkutano wa vijana mjini.

Bila ili wala lile, mama akanipa kibali bila kizuizi chochote maadamu alikuwa amenipenda kwa dhati. Alinitayarisha vyema na kunipa pesa za matumizi na baadaye akamwuliza rafiki yake mmoja aliyeishi mjini aniandalie makazi kwani hakutaka niwe nikilala kwenye msongamano. Maskini mama hakutambua kuwa nilikuwa naenda kujitafutia kifo.

Siku hiyo nilirauka asubuhi na mapema ili nijitayarishe kwenda. Nilikumbatiwa na mama akanipiga pambaja nilipokuwa nikiondoka na wote ndugu zangu wakanitakia heri njema. Nilimkuta msena wangu Bahati ameshifika katika mahali tulipokuwa tumefikiana. Tulisafiri kwa matwana moja ambayo ilikuwa na muziki uliozingoa ongoa roho zetu kwa midundo ya juu karibu izibue viwambo vya masikio yetu. Tulipofika, tuliwapata marafiki zetu tuliokuwa na uhusiano nao wanatungoja. Ama kweli hatukuwa tunaenda kwenye mkutano wowote ule wa vijana bali tulikuwa tumealikwa na masahibu hawa wetu tuwatembelee na kisha watutembeze mjini ili nasi tuujue. Tulipanda gari jingine na kuelekea mtaa mmoja nisiokumbuka jinsi walivyouita.

Baada ya gari hilo kuanza mwendo, nilishangaa kuona askari ambao walilisimamisha na kumwuliza dereva awashushe vijana wawili wezi ambao walikuwa kwenye gari. Ole wangu! Ilikuwa wale wapenzi wetu! Nilimwambia Bahati tunyamaze kimya kwani endapo tungeongea nasi tungetiwa mbaroni. Kunyamaza kwetu kulitutia mashakani kwani hatukujua tulikokuwa tunaelekea. Aidha hatukuwa na hela za kurudi nyumbani sote wawili. Mzee mmoja aliyekuwa ametuona alituarifu kuwa angetusaidia na malazi usiku huo kisha atupe nauli ya kurudi nyumbani siku iliyofuata. Tulikubali.

Usiku huo, mambo yalienda mvange, yaliyotendeka, ni methali kutaja hapa! Tuliambukizwa maradhi ya UKIMWI! Najuta vile nilijivika kilemba cha ukoka na hatimaye nikajipata katika janga hili lisilokuwa na tiba. Kweli majuto mjukuu, huja baadaye.

31. Kulingana na aya ya kwanza, "kuvalia ngozi ya kondoo" ina maana ya
A. kujifanya mjinga
B. kuwa mbwa koko
C. kujifunika ngozi ya kondoo
D. kujifanya mzuri ila wewe u mbaya

32. Mwandishi na Bahati walienda mjini
A. kwa tamaa ya kupata pesa
B. kuhudhuria kongamano la vijana
C. kuhudhuria mkutano wa vijana
D. kukutana na marafiki zao wa kiume

33. Mwandishi alirauka yaani
A. alimka asubuhi na mapema
B. alitoroka asubuhi na mapema
C. hakulala usiku kucha
D. aliruka kutoka kitandani

34. Mama yake mwandishi alichangia vipi katika kumwangamiza bintiye?
A. Kumfukuza nyumbani
B. Kumpa idhini ya kuenda mjini bila kutathmini
C. Kumpa ruhusa kuenda mjini bila kumpatia nauli ya kutosha
D. kumwita ndugu zake wampige pambaja kabla ya kuondoka

35. ..... kuzighilibu roho za watu; yaani
A. alifurahisha watu na kuwasifu
B. alichukia watu walimpenda
C. alipendwa na watu wengi kwa vitendo vyake
D. aliwadaganya watu wengi na kujionyesha kuwa mzuri

36. Vijana walikamatwa na polisi kwa sababu
A. walikuwa wezi
B. walikuwa walevi
C. walikuwa marafiki
D. hawakulipa nauli

37. Usemi "kilichotendeka gizani" lakini hatimaye kikawa wazi ni
A. tabia nzuri za Bahati
B. tabia za ndugu zake mwandishi
C. tabia mbaya za mwandishi
D. starehe za mbwa kukalia mkia

38. Ni methali gani inayotoa habari za aya ya mwisho?
A. Akiba haiozi
B. Majuto ni mjukuu
C. Bidii hulipa
D. Kikulacho ki nguoni mwako

39. Pesa za matumizi mtu anazotumia akiwa safarini huitwa
A. Nauli
B. Mshahara
C. Kiingilio
D. Masurufu

40. Kulingana na taarifa hii,
A. Wote walisaidiwa na mzee mmoja
B. Mwandishi na Bahati walitiwa mbaroni
C. Mwandishi na Bahati waliambukizwa Ukimwi
D. Wazazi wa mwandishi walijua njama ya mwandishi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Wakulima wawili walikuwa na mashamba ambapo walipakana. Si mashamba makubwa. Ni ekari moja moja tu. Mashamba yote mawili yapo kando kando ya njia kuu itokayo mjini. Shamba moja limelimwa vizuri sana.

Mahindi yamenawiri na kuvutia ajabu. Kila mpitajia hubung'aa pale na kuyakodolea macho. Hili, ni shamba la Bw. Mapato. Mapato hurauka asubuhi na mapema kushughulikia shamba lake. Bidii zake hizi alianza mapema tangu akilima. Alilima mapema, akapanda mapema na kupalilia mapema.

Wakati mvua ilipopungua, alitumia ndoo kuteka maji kutoka kwenye mto uliokuwa si karibu sana na shambani pake, akayanyunyizia mazao yake. Kweli juhudi ni pato.

Shamba la pili la Bwana Mzembe. Huyu ni rafiki shakiki wa usingizi na pombe. Kila hali shambani pake ni kinyume na shambani pa Bwana mapato. Mihindi imesinyaa. Mahindi machache na hafifu, kisha yanaliwa na ndege kila kitu si lolote si chochote pale shambani.

Mara akapita mhubiri mmoja. akaayaangalia mashamba yote mawili kwa zaidi ya dakika arubaini huku akiongea peke yake. Kumbe muda wote huo, Mapato ameketi katikati ya shamba lake kimya akimchuja mhubiri. Ilibidi asimame aulize kuna nini?" Alijibiwa kwa furaha na bashasha "Lo"! Mungu anakupenda, Mungu anakujua. Angalia alivyolifanya shamba lako lipendeze na kustawi . Hizi ni baraka za Mungu na ishara za jinzi, anavyokupenda!"

Mapato alicheka kidogo akasema, "ndugu mhubiri wacha uongo, wacha kupotosha watu. Mungu anampenda kila mtu. Mungu hutupangii kazi. sisi ndisi twamfanyia kazi. Ukijipenda na kuipenda kazi yako Mungu ataibariki. Mtenda kazi ni wewe si Mungu. Ukilala na kufanya kazi kivolaya Mungu atabariki nini? Waambieni watu ukweli."

41. Kulingana na aya ya kwanza si kweli kuwa
A. kulikuwa na wakulima wawili
B. mashamba yalikuwa madogo
C. kulikuwa na mashamba makubwa
D. mashamba yalilimwa na watu tofauti

42. Tukisema "kando ya"njia. "Kando ya" ni aina gani ya nena
A. kihisishi B. kihusishi
C. kielezi D. kiunganishi

43. Mashamba yote mawili yalikuwa
A. ya mtu mmoja
B. na mahindi mazuri
C. katika mazingira tofauti
D. na ukubwa sawa

44. Mahindi yaliwawiri. Hii ina maana kuwa
A. kuonekana yamenyauka
B. kuwa tayari kuvumwa
C. kuonekana na afya nzuri
D. yalikosa kupaliliwa kwa muda

45. Aliyenyunyizia maji shamba lake kulingana na kifungu hiki ni
A. Bw. Mzembe
B. Bw. Mapato
C. Mhubiri
D. Bw. Mzembe na Bw. Mapato

46. Kulingana na kifungu hiki mhubiri
A. aliliangalia shamba la Bw. Mapato pekee
B. alikuwa amealikuwa na Bw. Mapato
C. alikuwa amealikwa na Bw. Mzembe
D. alipitia kwa sadfa akienda zake

47. Mhubiri alizungumza na nani?
A. Bwana mzembe
B. Bwana mapato
C. Mtu mwingine
D. Peke yake

48. Mapato ana msimamo gani kuhusu ustawi wa mahindi shambani? Ni
A. baraka za Mungu
B. kulala shambani
C. umahiri wa mkulima
D. kuwa na ardhi nzuri

49. Mhubiri ana imani gani kuhusu mazao mazuri ya shamba la mapato?
A. Bidii zake
B. Mbegu njema
C. Mbolea ilitumika
D. Maombi kwa Mungu

50. Mapato unatoa mwito kuwa
A. huamini kila kitu tunachoambiwa
B. afanye kazi yake vizuri ndipo abarikiwe
C. ipo siku Mungu atamsaidia kila mtu
D. amtegemee Mungu hata kama ni mviv u